Programme des travailleurs d'établissement dans les écoles

# Vous accueillir, **avec plaisir!**




Huduma za mapokezi na usaidiai kwa wageni kwenye

District scolaire **francophone Sud**

*Apprendre. Grandir. Devenir.*

# BROSHA YA MPANGO WA SCHOOL SETTLEMENT WORKER (SSW)

## Dhamira

Ili kuwezesha ujumuishaji na ufanisi wa elimu wa wanafunzi wageni kwenye shule za DSFS na kuhimizwa ushiriki wao na ule wa familia zao katika maisha ya shule na jamii.



## Malengo

- Wanafunzi na wazazi/walezi wanafahamu zaidi mfumo wa shule wa kutumia Kifaransa wa New Brunswick na utamaduni wa Kanada
- Wanashiriki katika shughuli za shule na wanafahamu zaidi kuhusu rasilimali za jamii
- Wanaweka hali ya kuhisi kuwa mmoja wa jamii yao mpya
- Vijana wageni wanasaidia katika ufanisi wa elimu yao na maisha na mipango yao ya kazi
- Wazazi/walezi wanajumuishwa katika mambo yote ya jamii ya Kanada na wana stadi muhimu za kusaidia mipango ya elimu na kazi ya watoto wao
- Wafanyakazi wa shule wana uwezo na stadi za kusaidia ujumuishaji wa wageni katika mfumo wa shule

# SHULE YA DSFS NA RAMANI YA TIMU YA SSW

Timu ya SSW iko tayari kukukaribisha na kukuhudumia popote ulipo katika DSFS!





Financé par :

Immigration, Réfugiés et Citoyenneté Canada

Funded by:

Immigration, Refugees and Citizenship Canada

# WASILIANA NASI:

- Unataka kumwandikisha mtoto wako kwenye shule iliyo katika wilaya yetu?
- Unahitaji taarifa kuhusu mfumo wa shule?
- Una maswali au unahitaji usaidizi?
- Unataka kushiriki katika shughuli zetu?



**Wafanyakazi wetu wa kuwapa watu makao mapya wapo hapa ili kusaidia!**

Ili kuwasiliana na mwanatimu:
(506) 856-3333
Nouveaux.arrivants@nbed.nb.ca

francophonesud.nbed.nb.ca/nouveaux-arrivants/programme-tee

# HUDUMA ZINAZOTOLEWA NA SSW

Timu ya SSW inatoa huduma mbalimbali kwa wanafunzi wahamiaji na familia zao:

## Taarifa na maelekezo

- Usaidizi kwa wazazi wageni kwa usajili wa shule
- Vipindi vya taarifa kuhusu mfumo wa shule na maisha nchini Kanada
- Taarifa kuhusu mipango ya shule na shughuli za nje ya darasa
- Taarifa na usaidizi kwa vijana na wazazi zinazohusiana na upataji makao mapya na ujumuishaji katika maisha ya shule
- Rufaa za mzazi na familia kwa huduma na rasilimali zilizo katika shule na jamii
- Huduma za ufunzaji na uhamasishaji wa tamaduni mbalimbali kwa wazazi na wafanyakazi wa shule

## Miunganisho ya jamii

- Panga shughuli za jamii na utamaduni kwa vijana na familia zao ili kuwasaidia kugundua mazingira yao mapya na kuunda uhusiano na jamii yao
- Wasaidie vijana wageni kuwa washiriki wa mara kwa mara shuleni
- Unda nafasi za kushiriki na kufahamiana
- Himiza ushiriki wa vijana na familia katika shughuli za shule, nje ya darasa na jamii
- Fanya shughuli zinazoendeleza mazingira ya kuvutia na jumuishi kwa wanafunzi na familia



**Vous accueillir, avec plaisir!**

## Wewe ni mgeni kwenye New Brunswick na unataka kumpa mtoto wako:

- elimu bora
- kiwango cha juu cha uwili lugha
- shule ambayo ipo tayari kumkaribisha kila mtu na inaheshimu tofauti
- mazingira yanayokuza afya, usalama na hali njema

Timu ya SSW kwenye DSFS inatoa huduma za kukukaribisha na kuwezesha ujumuishwaji wako katika jamii ya shule.